**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

22/04/2024

# TANGAZO KWA UMMA

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA ANAWATANGAZIA WAKUFUNZI, WASIMAMIZI WA MAUDHUI, WASIMAMIZI WA TEHAMA NA MAKARANI WOTE WALIOSHIRIKI ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI LILILOFANYIKA MWAKA 2022 KUWA, AMEPOKEA VYETI KUTOKA OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS) KWA AJILI YA WASHIRIKI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022.

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU IMETOA VYETI KWA WASHIRIKI WOTE, KWA KUWA IMETAMBUA MCHANGO MKUBWA ULIOTOLEWA NA WASHIRIKI HAO KWA KUFANIKISHA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022.

KWA TANGAZO HILI, WAKUFUNZI, WASIMAMIZI WA MAUDHUI, WASIMAMIZI WA TEHAMA NA MAKARANI WOTE WA SENSA MNAJULISHWA KUFIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA SIKU ZA KAZI KUCHUKUA VYETI VILIVYOANDALIWA NA OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU KUANZIA TAREHE 22/04/2024 SAA 2:00 ASUBUHI HADI 9:30 ALASIRI.

WALENGWA WANATAKIWA KUFIKA NA KITAMBULISHO AU BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA OFISI YA SERIKALI YA KIJIJI AU KATA.

MWISHO WA KUCHUKUA VYETI HIVYO NI TAREHE 30/04/2024 SAA 9:30 ALASIRI, HIVYO WASHIRIKI WOTE MNASISITIZWA KUZINGATIA MUDA WA KUFIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA NGARA.

Josephati .M. Sangatati
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**

S.L.P. 30, Ngara, Simu 028 2226016, Nukushi 028 2226152, Barua pepe ded@ngaradc.go.tz, Tovuti www.ngaradc.go.tz